## Elimu ya teknolojia na mawasiliano

Ol pejeta inanuia kusaidia wanafunzi kujifunza ujuzi wa tarakilishi. Mwaka huu tuliweza kuwekea wifi, projekta na vifaa vya tablets kwa shule nane katika maeneo jamii ya hifadhi. Pamoja na hayo tuliweza kuajiri mtaalamu ambaye kazi yake ni kuhakikisha kuwa walimu katika shule hizi wanaweza kutumia vifaa hivi tulivyovinunua. Tunatumaini teknolojia hii mpya itaweza kuimarisha ubora wa elimu katika jamii yetu na kuwatayarisha wanafunzi vyema kwa maisha ya baadaye. Aprili mwakani tunatarajia kuongeza shule nane zingine.

*Washirika ni: Paul Allen & Family Foundation na Mawingu Networks.*



## Afya

Mwezi Julai 2016, Ol Pejeta iliweza kuwapatia wanajamii wasiojiweza huduma ya meno katika kambi ya meno na pia kuongeza uelewa kuhusu usafi wa meno. Haya yote yalifanyika katika shule ya msingi Matanya.

Mamia ya wanakijiji kutoka Njoguini, Chuma, Mirera, Marura na Sweetwaters walijitokeza kufaidika na huduma hii. Zaidi ya huduma hii ya meno, Ol Pejeta pia huweza kutekeleza huduma za kliniki kila mwezi kusaidia jamii za Debatas, Tanki Nyeusi, Ereri na Endana kule kaskazini.

*Washirika ni: Consolata Mathari hospital and Nanyuki General Hospital.*

## Mawasiliano Kupitia Ujumbe Mfupi (sms)



Hivi majuzi Ol Pejeta ilizundua namba ya kutuma ujumbe mfupi. Hii inapatia jamii fursa ya kuwasiliana moja kwa moja na community department ya Ol Pejeta kwa mawasiliano na maoni. Nambaa hii ni ya ujumbe mfupi tuu.

Ukiwa na ujumbe wowote kuhusiana na ufadhili, uwindaji haramu, malalamiko au maoni, tafadhali tuma ujumbe mfupi kwa namba hii 0790889940. Kama ungependelea kupokea ujumbe kuhusu nafasi za ufadhili, nafasi za kazi, miundo mbinu ya nishati, kilimo na mengine, tafadhali tuma ujumbe mfupi wenye jina lako na kijiji chako kwa 0790889940.

## Uasidizi kwa wakulima

Mpango wa 'Full Basket' ni mradi ambao unalenga kuboresha usalama wa chakula na maisha bora katika jamii zinazoizunguka hifadhi ya Ol Pejeta. Mradi huu unakuza kilimo cha kisasa ukizingatia teknolojia ya umwagiliaji; kilimo cha 'greenhouse' bila kusahau uvunaji wa maji ya mvua eneo la Tigithi na Lamuria.

Tarehe 14 Aprili Ol Pejeta iliwezesha mkutano katika kijiji cha Lamuria ambao ulihudhuriwa na mamia ya wakulima ambao waliweza kubadilishana mawazo na kujifuza mbinu mpya za kuongeza ubora wa mazao yao. Katika shughuli hii wakulima waliweza kukutana kwa mazungumzo na wafanyakazi kutoka benki ya Equity, Biashara Sacco, Wizara ya Kilimo, OSHO, VegPro, wakulima wa kibiashara na Sygenta. Vile vile walikuwemo viongozi kama vile Joel Nyaga ACC Lamuria, machifu wa Lamuria na Tigithi na mdogo wa chifu eneo la Mutaro. Pia tulikuwa na wawakilishi wetu kutoka Tharua, Ngobit, Chuma, Riachu, Mwakinya, na Weruini. Zaidi ya watu 128 walihudhuria siku hii ya kufana.

*Washirika: British Airways, Flora & Fauna International*






OL PEJETA
CONSERVANCY



# JARIDA LA WANAJAMII

NOVEMBER 2016

## Uzalishaji Kwa Njia ya Mipira

Bwana Samuel Gikunju ni mkulima mdogo kutoka eneo la Withare. Hapo awali alikuwa akidhani kuwa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa wa kisasa ni wa wakulima matajiri pekee. Mwaka wa 2011, aligundua huduma nafuu ya upandikizaji bandia iliyokuwa inatolewa na hifadhi ya Ol Pejeta na akaaamua kuijaribu huduma hii na kwa sasa anavuna faida ya hali ya juu. Wale ng'ombe asilia aliokuwa nao awali walikuwa wanampatia maziwa kiasi cha lita nne kwa siku, hawa ng'ombe wawili wa kisasa wanampatia lita arobaini za maziwa kila siku. Anakiri kuwa ameweza kujiwekea akiba ya fedha kwa ajili ya kuzuia na kutibu magonjwa. Pia ameweza kuanza mtindo wa kufungia ng'ombe hawa na kuwapatia chakula katika makao yao (zero-grazing) mfumo ambao unapunguza kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira na pia kupunguza hasara wakati wa ukame.



## Elimu: Ufadhili wa Ol Pejeta

Hifadhi ya Ol Pejeta pamoja na washirika wengine hutoa udhamini kamili wa kitaaluma na sehemu ya ufadhili kila mwaka. Kwa sasa tuna wanafunzi 57 na huwa tunachukua wengine punde tu wale walio mbele wanapokamilisha masomo yao ya shule ya upili.

### Ni nini tofauti kati ya ufadhili kamili na sehemu ya ufadhili?

Ufadhili kamili huwa unapatikana kila mwanzo wa mwaka kwa wale wanafunzi wasiojiweza katika jamii yetu. Ufadhili huu unagharamia ada yote ya shule ya mwanafunzi huyu kwa kipindi chote atakachokuwa katika shule ya upili. Ibainike kuwa ufadhilii huu hautogharamia nauli na vifaa vyovyote vitakavyohitajika shuleni kama vile sare za shule ambazo wazazi na walezi watahitajika kugharamia. Sehemu ya ufadhili nayo ni kiasi kidogo cha pesa kinachotolewa kuwasaidia wanafunzi wanaosumbuka na ulipaji wa ada.

### Nawezaje kuomba ufadhili huu?

Kila mwanzo wa mwaka fomu za ufadhili hupatikana kwa wawakilishi wetu wa jamii ambao huweza kuzisambaza katika shule mbalimbali. Ol Pejeta pia huwatumia ujumbe mfupi wale wote walio na mawasiliano nao kuwajulisha kuwa fomu hizo zinapatikana. Nafasi ni chache hivyo basi ufadhili hutolewa kwa wale walio na haja ya juu zaidi.



### Jinsi ya kutuma ombi la ufadhili:

#1 Muulize mwakilishi wa jamii yako kutoka Ol Pejeta akupe fomu ya maombi
#2 Jaza fomu hiyo ukitoa maelezo yote yanayohitajika
#3 Rudisha fomu hiyo kwa mwakilishi wako pekee
#4 Andika ujumbe mfupi kwa Ol Pejeta ukitumia namba uliyopewa, ambatanisha jina lako na sehemu unayoishi katika ujumbe huu
#5 Ol Pejeta watakusanya fomu hizi na pamoja na viongozi wa maeneo kuwachagua wale wanaostahili zaidi.

### Matarajio yetu:

#1 Kuwa jamii itatusaidia katika kuchagua wale wanaostahili zaidi
#2 Kuwa wanafunzi watawasilisha matokeo yao kwa wawakilishi wetu kila mwisho wa muhula.
#3 Wanafunzi ni lazima wapatikane kila likizo kwa mazungumzo kuhusu taaluma na matokeo yao wakiwa na wazazi wao na wafanyakazi wa Ol Pejeta.
#4 Ol Pejeta ina haki ya kusitisha ufadhili endapo mwanafunzi atashindwa kudumisha kiwango cha kutosha kitaaluma na kinidhamu.

